TANGAZO LA SERIKALI NA. 734 la tarehe 23/8/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA IBULYU YA MWAKA, 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa eneo la Ibulyu ya mwaka, 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (Mpango wa Urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa halmashauri ya wilaya ya Bariadi.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IB6 yenye majira – nukta 604085MS, 9693661KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS149$^{0}$7’13”MS kwa umbali wa kilomita 0.95 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IB7 yenye majira – nukta 604575MS, 9692842KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS203$^{0}$41’42”MG kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IB1 yenye majira – nukta 604374MS, 9692384KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ273$^{0}$34’9”MG kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IB2 yenye majira – nukta 603877MS, 9692415KZ;

baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KS0$^0$0'0"MG kwa umbali wa kilomita 0.26 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IB3 yenye majira – nukta 603877MS, 9693678KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa KZ306$^0$54'44"MG kwa umbali wa kilomita 0.5 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IB4 yenye majira – nukta 603350MS, 9693098KZ; baada ya hapo mpaka
unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ44$^0$13'16"MS kwa umbali wa kilomita 0.35 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IB5 yenye majira – nukta 603704MS, 9693463KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ62$^0$32'23"MS kwa umbali wa kilomita 0.38 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
14 Agosti, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*